

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Anwani ya simu: "UTUMISHI", DSM.
Simu Nambari: 2118531/4
Nukushi: 2125299
Barua pepe: permsec@utumishi.go.tz



Ofisi ya Rais,
Menejimenti ya Utumishi wa Umma,
Jengo la Utumishi,
8 Barabara ya Kivukoni
S.L.P. 2483,
11404 DAR ES SALAAM.

Kumb. Na.CAC.17/22/01/T/34

22 Septemba, 2015

WARAKA WA UTUMISHI NA. 1 WA MWAKA 2015

**UTARATIBU WA MALIPO YA POSHO YA KUKAIMU CHEO CHA
MADARAKA (SUPERLATIVE SUBSTANTIVE POST)**

1.0 Utangulizi

1.1 Utaratibu wa kukaimu nafasi za Madaraka (Superatibe Substative Posts) umeelezwa kwenye Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma Toleo la Mwaka 2009, hususan Kanuni D.18 – D.26. Watumishi wanaoteuliwa kukaimu nafasi hizo hulipwa Posho ya Kukaimu nafasi za Madaraka. Kwa Mujibu wa Kanuni L.15 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, Toleo la Mwaka 2009, posho ya kukaimu madaraka hulipwa kwa kuzingatia tofauti ya mshahara wa cheo kinachokaimiwa na mshahara wa cheo cha mtumishi anayekaimu.

1.2 Kwa Mujibu wa Kanuni hizi, kuna aina mbili za kukaimu nafasi za Madaraka ambazo ni:-

- (i) Nafasi zinazokaimiwa kwa muda mfupi kutokana na wahusika kuwa wagonjwa, safarini, likizoni, masomoni, n.k.
- (ii) Nafasi wazi zinazokaimiwa zikisubiri kukamilika kwa mchakato wa uteuzi wa kuzijaza rasmi.

2.0 Utaratibu Uliopo wa Kukaimu Nafasi za Madaraka

2.1 Kwa Mujibu wa Kanuni zilizoainishwa katika aya 1.1 ya Waraka huu, malipo ya posho hiyo hulipwa kupitia Kifungu cha Matumizi Mengineyo (Other Charges – OC).

2.2 Pamoja na maelekezo yaliyopo katika Kanuni hizi za Kudumu kumekuwepo madai mengi ya malimbikizo ya posho ya kukaimu nafasi za madaraka kutoka kwa Waajiri mbalimbali katika miaka ya hivi karibuni, kwa kuwa Waajiri hushindwa kulipa posho hizo kwa kutumia fedha za Matumizi Mengineyo kutokana na ufinyu wa

